**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI (OWM-TAMISEMI)**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO**

**Namba za simu**

Mkuu wa shule : **0754078905**

Makamu Mkuu wa Shule: **0768438601**

Email:

SHULE YA SEKONDARI ICHWANKIMA,

S.L.P 81,

**CHATO- GEITA.**

---

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ……………………………

S.L.P …………..

…………………

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ICHWANKIMA HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO MKOA WA GEITA MWAKA ………….

Ninayofuraha kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka ………. tahasusi ya HGL/PCB. Nakupongeza karibu sana Ichwankima.

Muhula wa masomo unaanza tarehe ………….. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ………….. Mwisho wa kuripoti ni tarehe ……….. Ukifika shuleeni utapokelewa na makamu mkuu wa shule na kusajiliwa .

MAHALI SHULE ILIPO.

Shule ya sekondari Ichwankima ipo katika wilaya y Chato katika Mkoa wa Geita kata ya Ichwankima kijiji cha Imalabupina. Kuna umbali wa kilometa 25 kutoka makao makuu ya halmashauri ya wilaya ya Chato.

NAMNA YA KUFIKA SHULE YA SEKONDARI ICHWANKIMA.

1. Kwa wanaoanzia safari zao Mwanza wanapanda mabasi yaendayo Bukoba au yanayoishia Muganza na kuteremka kituo cha Nyamirembe
2. Kwa wanaotoka Dar es Salaam ,morogoro, Dodoma, Singida au shinyanga wapande mabasi ya kwenda bukoba ,wakifika runzewe watapanda magari ya kwenda Bwanga na wakifika Bwanga watapanda magari ya kwenda Bukoba au Muganza na kuteremka kituo cha Nyamirembe.
3. Kwa wanaotookea karagwe kupitia Bukoba watapanda magari ya kwenda mwanza watateremka kituo cha Nyamirembe.
4. Kwa wanaotoka kigoma watapanda mabasi yaendayo mwanza kupitia runzewe wakifika Bwanga watapanda magari yaendayo muganza na kutelemka kituo cha nyamirembe**.**

5. Kwa wanaotoka ngara kupitia Biharamulo wakifika biharamulo watapanda magari madogo yaendayo chato au muganza na kutelemkia kituo cha Ichwankima sekondari.
   NB. Wote watakaotelemkia kituo cha Nyamirembe chukua usafiri wowote kuelekea mahali **shule** ilipo.

**2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

2.1 Sare za shule

a. Sketi mbili ndefu(2) zenye rangi ya daka grini( dark green)( Istimu no.1)

b. Hijabu nyeupe(kijuba) kwa waislamu

c. Tai dark green

d. Shati mbili(2) nyeupe mikono mirefu

e. Sweta kijivu yenye V

f. kiatu cheusi chenye kamba

g. Soksi nyeupe ndefu

h.Tshirt moja rangi ya kijivu yenye kola

i. Nguo za kushindia(shamba dress) – Gauni mbili(2) rangi ya dark blue(Istimu no.1)

j. Tracksuit (suruali najaketi lake rangi ya dark blue) sare ya kuvaa wakati wa masomo ya usiku

k. Sare za michezo- tracker Maloon, raba na soksi

2.2 Michango ya shule

a. Michango yote ilipwe kwenye akaunti Na. ICHWANKIMA SEKONDARY SCHOOL RECCURENT ACCOUNT; Ac. No; 32701200070 NMB.( Tafadhari andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip)
   i. Shilingi 65,000/=kwa ajili ya uendeshaji
   ii. Shilingi 5,000/= kwa ajili ya tahadhari
   iii. Shilingi 5,000/= kwa ajili ya nembo.
   iv. Shilingi 5,000/= kwa ajili ya kitambulisho

   JUMLA KUU NI TSH. 80,000/=

NB. Jukumu la matibabu kwa mwanafunzi ni la mzazi/mlezi , hivyo mzazi/mlezi anashauriwa kumtafutia mtoto wake bima kwa ajili ya kupatiwa matibabu kwa muda awapo shuleni.

b. Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni;
   1. MCHEPUO WA (HGL)
   - Fyekeo, squizer, jembe na mpini wake na mfagio wachelewa,ndoo ya chooni na kopo lake,ndoo moja ya lita 20.
   2. MCHEPUO WA (PCB)
   - Fyekeo, soft broom, mopa,hard broom, jembe na mpini wake, ndoo ya chooni na kopo lake nan doo moja ya lita 20.

Mahitaji binafsi.

- Godoro futi mbili na nusu
- Chandarua pembe nne rangi nyeupe
- Ndoo mbili moja yenye ujazo wa lita 20 na moja lita 10.
- Chombo chenye ujazo wa lita 5 cha kuhifadhi maji ya kunywa
- Bakuli, sahani,kikombe na kijiko kwa ajili ya uji na chakula.
- Kalamu za kutosha na vifaa vya kuchorea
- Flatfile kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu zako.
- Counterbooks 12 za 4 quire au 3 quire
- Ream 1 A4 double A
- Oxford advanced learners dictionary kwa matumizi yako
- Scientific calculator
- Hati maalumu ya vipimo vya daktari kuthibitisha hali ya Afya yako. (fomu imeambatanishwa)
- Dissecting kit kwa wanafunzi wa mchepuo wa PCB.
- Mashuka jozi mbili rangi ya pink, blanket moja, foronya moja.

2.3 MAVAZI NA NGUO BINAFSI

> Jozi moja ya kanga

> Taulo

> Kanda mbili za kuogea

> Nguo za kulalia

> Underskirts mbili au zaidi na nguo za ndani zisizopungua 12 na pads bunda 5.

3. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

a. Wizi

b. Uasherati na ushoga

c. Ubakaji
d. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
e. Kupigana na kupiga
f. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
g. Kudharau bendera ya Taifa
h. Kuolewa /kuwekwa kimada
i. Kupata mimba/kutoa mimba
j. Kugomea adhabu kwa makusudi
k. Kuwa na simu ya mkononi
l. Kutumia vifaa vya umeme kama jagi au heater ya kuchemshia maji,pasi

m. Kutumia vipodozi vya aina yoyote
n. Kununua au kuingiza vyakula vya aina yoyote bila ruhusa ya mwalimu
o. Udanganyifu wa aina yoyote katika mitihani

4.SHERIA ZA SHULE

a. Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakaziwote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b. Mahudhurio katika shughuli zote ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni jambo la lazima.
c. Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
d. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
e. Kutunza usafi wa mwili ,mavazi na mazingira ya shule.
f. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
g. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
h. Kutunza mali za umma.
i. Kusimama na kusalimu walimu na watu wazima.
j. Kupanga mstari wakati wa kupokea huduma.

5.Viambatanisho na fomu muhimu

a. Fomu ya uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya serikali

b. Fomu ya mzazi/mlezi kukiri kukiri kukubaliana na sharia na taratibu za shule

Unatakiwa kutii sharia ,taratibu na kanuni za shule muda wote uwapo shuleni. Kutojua sharia za shule haitakuwa kinga ya kutokuchukuliwa hatua.

……………………………………….

ELIWAKO MDUMA ANDERSON

MKUU WA SHULE

Mawasiliano: 0754078905

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI ICHWANKIMA